TIMER NATIONAL SERIES
MAJARIBIO YA MTIHANI
DARASA LA NNE KISWAHILI {4}

Toleo la: 0092014

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO *Muda: Saa 1 dakika 40*

1. Umepewa kijitabu cha maswali na karatasi ya kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

JINA LAKO **JINA LA SHULE YAKO**

Soma kifungu hiki ukijaza nambari 1-15.

Wawindaji haramu wanaharibu uchumi __1__ nchi yetu. Wao __2__ wanyama wa pori. Wanyama __3__ wanaletea nchi yetu pesa na pia __4__ huja nchini __5__ kuwaona wanyama hawa.

Siku __6__ wawindaji hawa walikuwa __7__ kazi yao haramu. __8__ walikuwa msituni __9__ wawindaji hawa na __10__ mbali waliwaona watu. Walipofika __11__ nao, waliona kuwa walikuwa majangili.. __12__ wameangamiza ndovu __13__. Waliwashika na __14__ silaha zao __15__.

	A	B	C	D
1.	ya	wa	la	za
2.	wanawa	wanawauwa	wanaua	wanawaua
3.	hizi	huyu	hawa	haya
4.	wakimbizi	watalii	watoro	walowezi
5.	mwetu	yetu	letu	mwetu
6.	moja	mmoja	mumoja	monja
7.	kwa	na	katika	kwenye
8.	Maaskari	Mapolisi	Polici	Askari
9.	wakiwaficha	wakiwatafuta	wakiwalinda	wakiwasumbua
10.	kwa	na	na	mwa
11.	mbali	kando	nyuma	karibu
12.	Walikua	Hawakua	Walikuwa	Hawakuwa
13.	mawili	mbili	miwili	wawili
14.	kuwanyaganya	kuwanyang'anya	kuwapa	kutupa
15.	sote	zote	yote	lote

Kutoka swali la 16-30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo.

16. Juma ni _____ kuliko Yohana.

A. safi B. nzuri

C. mhodari D. msafi

17. Ni nini maana ya alama hii ya barabarani?



A. Vituta

B. Ilani

C. Matuta

D. Hospitali

18. Mwezi wa tano wa mwaka huitwa _____.

A. Mai B. Meyi

C. Aprili D. Mei

19. Mpunga ni mmea unaotupa _____.

A. ndizi B. kahawa

C. mchele D. sukari

20. Ni nini kinyume cha jogoo? _____

A. Koo B. Kuku

C. Jiimbi D. Pora

21. Mzoga wa mbwa unanuka _____.

A. fyu! B. fye!

C. fe! D. pu

22. Umbo hili ni gani?



A. Sambasamba

B. Tufe

C. Wimbi

D. Zigizagi

23. Kamilisha methali:

Bendera hufuata _____.

A. mlingoti B. baridi

C. upepo D. hewa

24. Ni ndege yupi kati ya hawa ambaye hufugwa nyumbani?

A. Heroe B. Njiwamanga

C. Sigi D. Korongo

25. Ni vazi lipi si la ndani?

A. Kazibao B. Chupi

C. Kocho D. Kanchiri

26. Tumia -ote- kwa sahihi.

Watu _____ wamekuja.

A. wote B. yote

C. zote D. sote

27. Sijamwona simba ____ macho yangu.

A. kwa B. ya

C. na D. ni

28. Andika kinyume.

Mchana ____.

A. jua B. mwangaza

C. usiku D. adhuhuri

29. $^1/_6$ huitwa ____.

A. subui B. sudusi

C. tusui D. humusi

30. Gari la Mzee Sonko ni _____.

A. lipya B. mpya

C. ipya D. jipya

Soma makala haya kisha ujibu maswali 31-40.

Nyumba ya kina Petro inapendeza sana. Nyumba yenyewe ni ya mawe na ina chumba cha wageni, mbali na sebule, stoo, vyoo na vyumba vya kulala vitatu.

Sebuleni, kuna sofa za rangi ya samli iliyochukuana na rangi ya kuta. Mazulia ni ya yangi ya kahawia ambayo ndiyo rangi ya meza ya katikati na stuli zake. Juu ya rafu, kumewekwa vitu vya kitamaduni kama vile kawa na vibuyu. Runinga ipo pembeni juu ya kabati maalumu iliyoundwa kuchukua mahitaji mbalimbali ya runinga. Kinanda, ingawa kingali kinafanya kazi, hakitumiki sana.

Picha mbalimbali za familia zimeangikwa katika viambaza. Kwenye madirisha, kuna pazia za rangi ya kahawia. Feni iko katikati ya dari ikijaribu kuburudisha chumba wakati wa joto. Katika kabati, kumewekwa vitu vidogo vidogo vinavyohitajika mara kwa mara hasa kama vikombe, sahani, gilasi na vifaa vya huduma ya kwanza.

31. Makala haya yanazungumzia juu ya nyumba ya akina nani?
    A. Kamau B. Akinyi
    C. Petro D. Kamene

32. Nyumba yenyewe ina vyumba vingapi?
    A. 2 B. 3
    C. 5 D. 7

33. Rangi ya kuta ni rangi gani?
    A. Samli B. Nyekundu
    C. Nyeusi D. Nyeupe

34. Neno jingine lenye maana sawa na sofa ni lipi?
    A. Kochi B. Zolia
    C. Rafu d. Dari

35. Rangi ya meza ya katikati ni ipi?
    A. Samawati B. Nyekundu
    C. Kahawia D. Nili

36. Viambazani kuna nini?
    A. Sahani B. Runinga
    C. Picha D. Kinanda

37. Vibuyu vimewekwa wapi?
    A. Kabatini B. Juu ya rafu
    C. Jikoni D. Sebuleni

38. Kazi ya feni ni ipi kulingana na ufahamu?
    A. Kuburudisha chumba wakati wa joto.
    B. Ni gari.
    C. Ni chakula.
    D. Sijui.

39. Kati ya vitu hivi, ni kipi ambacho hakijawekwa kabatini?
    A. Vikombe B. Kinanda
    C. Sahani D. Gilas

40. Kichwa mwafaka cha hadithi hii ni?
    A. Sebuleni
    B. Matumizi ya feni
    C. Vyumba vya watoto
    D. Nyumba inayopendeza.

Soma barua hii kisha ujibu maswali 41-50.

Shule ya msingi ya Soma,
Sanduku la posta 221,
MWAKIZONI,
15-09-1964.

Kwa rafiki Jeffa,

Natoa salamu nyingi sana kutoka kwetu hapa mjini. Wewe hujambo hapo ulipo? Je, masomo yanaendeleaje? Hapa tunafanya bidii sana katika masomo yetu. Dada anajitayarisha kwa mtihani wake wa darasa la nane.

Mimi na dada yangu tunasoma ili tusishindwe na wenzetu darasani. Mwisho wa muhula uliopita nilishikilia nafasi ya tatu. Baba, mama na wajomba wote walifurahi sana. Walinipa zawadi. Wasalimie wazazi, ndugu na marafiki zao. Tafadhali niandikie barua upatapo waraka huu.

Ni rafiki yako,
Kalama Sindio

41. Barua hii iliandikwa na nani?
A. Kola B. Jeffa
C. Dada D. Kalama

42. Jina la mji ulioko karibu sana na mwandishi ni ___
A. Kalama B. Mwakizoni
C. Jeffa D. Kibao

43. Unafikiri kuwa barua hii iliandikwa muhula gani?
A. Wa pili B. Wa tatu
C. Wa kwanza D. Septemba

44. Kalama alipewa zawadi na nani?
A. Baba, mama, shangazi
B. Mama, shangazi, wajomba
C. Shangazi, mama, mjomba
D. Wajomba, mama, baba

45. Jibu la hujambo ni?
A. Marahaba B. Sijambo
C. Hatujambo D. Mzuri

46. Ni nani anayejitayarisha kufanya mtihani wa darasa la nane?
A. Kola B. Dadaye Jeffa
C. Dadaye Sindio D. Kalama Sindio

47. Jina jingine la barua kulingana na taarifa hii ni _____
A. anuani B. muhula
C. bidii D. waraka

48. Kulingana na taarifa, Sindio _____
A. anafanya bidii.
B. ni mzembe.
C. anaburura mkia.
D. ni mjinga.

49. Mwandishi alikuwa nambari tatu lini? Mwisho wa muhula wa ____
A. kwanza
B. pili
C. tatu
D. mwaka

50. Taarifa hii ni mfano wa _____
A. hotuba
B. barua rasmi
C. shairi
D. barua ya kirafiki